*Jiwe la kujengea No:29*

# BARAKA ZETU ZA UKOMBOZI NI KUPITIA USHINDI WA MSALABA

**Yohana 19:30; Basi Yesu alipokwisha kuipokea ile siku alisema, imekwisha, akainama kichwa akaisalimu Roho yake.**

Siku zote nimesema, nimekutana na watu wa aina mbili wanaosoma maanndiko na kuweka akili zao na Wapentekonte hao wanaosoma maandiko na kuweka akili zao kimsingi wanasoma maandiko na kuweka mawazo yao na kusema vema Sisi ni wana wa Mungu wanaamini hilo - Ndiyo, ndiyo Bwana hawana Imani katika hilo lakini Wapentekonte wana wa Mungu ni kama mtu alie na pesa Benki na hawezi kuandika cheki na yule mwingine anaweza kuandika cheki lakini hana pesa Benki kama ungeweza kufanikiwa kuwaweka pamoja, mpaka Wanaume na Wanawake wakatambua na ile ishara ya kuonyesha ***(Kutoka 12:13)*** mnayo haki kwa kila baraka ya ukombozi ambayo Mungu aliahidi. Kila kitu alicho ahidi cha kwenu, shikilia ishara yako katika Imani yako isiyoyumba hapo unapoomba na katika neno lake Imani katika Neno Lake (1).

Sasa pia tunaona katika ***(Waebrania 12:24)*** kwamba Agano jipya, ile damu inazungumza mambo mazuri, ile damu inanena kwa hiyo damu ina sauti na sauti ya damu ni Neno Haleluya. Hiyo ndiyo inayoifanya iwe sahihi au iwe makosani lile neno linatambulishwa na sauti ya damu, ile sauti ya damu na inaleta uhai kwenye neno na klihuisha hilo ***(Warumi 8:11)*** Amina, amina, amina. Hakika ile damu inazungumza mambo mazuri lile agano la kale damu ilizungumza juu ya hatia katika agano jipya inazungumzia ukombozi katika agano la kale inazungumzia mauti na huzuni katika agano jipya inazungumzia juu ya ufufuki na uzima inazungumzia unzima, inazungumzia Mbingu, na damu ile ile ambayo imemwagika kwenye ardhi ile ambayo ilimuita ndugu yake aliekufa au iliyomuita ndugu yake ambaye amemuua yeye ***(Mwanzo 4:8-12)*** damu ya Yesu Kristo inafunika dhambi zetu zote inazungumzia amani na Ufufuko na nguvu na uzima na uponyaji na Baraka zote za ukombozi ambazo damu ilimwagika kwaajili yake inatuzungumzia sisi hakika ile damu inazungumza (2).

Sasa kumbuka kila baraka yoyote ya Ukombozi imeshanunuliwa ile gharama imelipwa kuna njia moja tu ambayo wewe unaweza ukaipata hiyo ni kuiamini hiyo yeye ni kuhani mkuu wa maungano yetu, ***(Waebrania 4:14-16; Waebrania 7;18-19)*** kwa hiyo awezi akafanya chochote kwaajili yetu mpaka kwanza tumekubali hicho na halafu tunapokiri hicho hapo sasa yeye ni kuhani mkuu, muombezi anaenda kumtuma katika hilo na kulifanya liwe sahihi kwa hiyo tunaomba na kuamini leo kwamba katika ukarimu wake na rehema zake kwamba atatupa sisi kwa wingi wa Neema zake na sasa kumbuka ni lazima ulikubali hilo ***(Yohana 1:12-13)*** (3)

Ni Roho Mtakatifu leo akilinda Mioyo yetu iliyo mwaminifu ambayo itaamini ujumbe kila kitu katika Biblia ambacho kimeahidiwa ni kwaajili ya muaminio na unapoikubali he kitambulisho kwa hilo na halafu kila ahadi iliyoahidiwa na miliki yako na Roho Mtakatifu yupo pale kulihuisha hilo kwako kazi nifanyazo na wewe utazifanya ***(Yohana 14:12)*** hizi ishara utafuatana nao waaminio ***(Marko 16:17)*** huo ndyo uthibitisho tunapoona kundi la watu limekaa pamoja na hi zi ishara zinajidhihirisha zenyewe hiyo ni ushahidi kwamba Mungu ameweka ushuhuda pale

kuthibitusha kwamba huyo ni mali ya Mungu Amina. Tayari tumeshafufuka kutoka kwenye mambo ya Dunia kwenda kwenye mambo ya ahadi za Mungu siyo tuta ni tayari hiyo ni uthibitisho kwamba ipo pale na wakati Roho wa Mungu anapokuja juu yako na wewe kwa kweli ni moja wa sifa za Mungu ambazo alizinena juu yake sasa kama bado utashangaa na kujishangaa na kwenda hapa na pale na kila kitu kinginesho na kamwe hutakuja kwenye maarifa ya kweli ***(2Timotheo 3:7)*** kama wewe ni mmoja wa hawa mambo ya kule yanapita haraka sana unaona? nawe unakua mpya na mpango wa ukombozi unakuwa umemalizika uko tayari kutii kila neno ambalo Mungu amelizungumza juu yako. Unaona? Kwaajili yako kulitenda wewe unaluwa mtu mjemi hatimiliki ni yako, madeni yote yamelipwa, yote yamefutwa inakua kama ilivyokuwa siku ya Pentekoste. (4)

Imani ni ushindi juu ya mauti, imani ni ushindi dhidi ya dhambi, Imani ni ushindi dhidi ya magonjwa, Imani ni ushindi dhidi ya mashaka, Imani ni ushindi juu ya wasiwasi, Imani ni ushindi juu ya Dunia ***(1Yohana 5:4)*** (5)

Sasa ni kitu gani kilitokea kwenye Msalaba wa Kalvari? katika Yesu Kristo tuna ukombozi kupitia damu yake, Msalaba wa dhambi, kutokana na utajiri wa Neema yake ***(Waefeso 1:7;*** Wakolosai 1:14 ; Waebrania 9:11-12) alituosha sisi kutoka dhambi zetu kutoka damu yake mwenyewe ***(Ufufuo 1:5; Yeremia 31:34; Isaya 43:25)*** na ametusamehe maovu yetu yote ***(Zaburi 103:1-3)*** jambo moja kuu muhimu ambalo Kalvari ilimaanisha kwetu na kwa Dunia ni ilimaliza swala la dhambi mara moja kwa wakati wote ***(1 Yohana 3:9; 1Yohana na 5:18 ;1 Petro 1:18-19; Warumi 8:34)*** Yesu Kristo ametukomboa sisi kutoka kwenye laana ya sheria kwa yeye kufanyika laana kwa ajili yetu kwa maana imeandikwa amelaaniwa yeyote amngikwaye mtini ili baraka za Abrahimu ziweze kuja kwetu sisi (watu wa mataifa) kupitia Yesu Kristo ili ziweze kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya Imani ***(Wagalatia 3:13-14).***

Yesu Kristo aliifuta ile hati ya deni ya dhambi iliyokuwa inatustaki sisi alilipa deni letu ambalo lilikuwa linatuelemea sisi na lichukua akaiondoa kwetu akiigongomelea kwenye Msalaba wake ***(Wakolosai 2:14).***

Yesu Kristo alilipa ile adhabu ya dhambi ile gharama ya dhambi ilimalizika, mshahara wa dhambi ni mauti ***(Warumi 6:23)*** mwanadamu alionekana kuwa na hatia ya dhambi na dhambi ilikuwa ni adhabu ambayo mtu asingeweza kui;ipa ***(Warumi 3:23-27)*** ile adhabu ilikuwa kuu mno mpaka hakukua na mtu yeyote ambaye angeweza kulipa hiyo adhabu kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu ***(Warumi 3:23-24)*** sisi sote tumezaliwa katika dhambi, tukaumbwa katika uovu, tukaja Duniani tukisema uongo ***(Isaya 64:6; Warumi 3:4)*** kwa hiyo hakukua na hata mmoja wetu sisi ambaye angestahili kwa hiyo aliweza kulipa ni Mungu mwenyewe akiwa ndani ya Mungu alionja mauti kwa kila mmoja ***(Waebrania 2:9)*** yale maneno yatatendeka tuko huru na kifo maana yake ni kutenganishwa na Mungu aliteseka badala yetu kule kutengana kwa kutisha kutoka kwa Baba pale alipolia Mungu wangu' Mungu wangu mbona umeniacha mimi ***(Mathayo 27:46)*** yeye mtu asiyejua dhambi alining'inizwa pale kama mtu asiye na Mungu kama mwenye dhambi mchoyo ili tuweze kuona kamwe hatashindw wala kutuacha sisi ***(Isaya 53:6; Ezekiel 18:20 : Warumi 6:23; Waebrania (13:5-6 ; Warumi 8:38-39)*** Biblia ilisema adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake ***(Isaya 53:5)*** hii adhabu ilikua ni nini marudi? Mateso yake ya uchungu na kifo Yesu Kristo alichukua hukumu yetu juu yake ile hasira ya Mungu iliyo mwagwa juu yake mpaka akaonja mauti badala

yetu Biblia inasema mshahara wa dhambi ni mauti. Yesu alilipa hiyo gharama kuu kwa ajili yetu. Hiyo gharama ilikuwa ni nini? Damu iliyo ya dhambi sana isiyochafuliwa mwanaye kondoo ilikuwa ni damu ya Mungu mwenyewe. Yesu Kristo kama kondoo wa Mungu alimwaga damu yake Takatifu damu ya kiungu kama mwana kondoo ***(Yohana 1:29)*** Mungu mwenyewe alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake Yesu alifanya dhambi kwa ajili yetu ***(2Wakoritho 5:18-27)*** katika agano la kale gharama ilikuwa damu isiyo na hatia ya mnyama ingawaje bado kulikuwa hakuna kufunguliwa na hiyo lakini ilikuwa tu kifuniko cha aliyetenda dhambi ***(Waebrania 9:12-14) (1Petro 2:22-24:Ezekiel 18:20)*** lakini Yesu alionja mauti kwa kila mmoja wetu ***(Waebrania 2:9)*** mauti yake Yesu yaliharibu mauti yenyewe na yakaleta uhai na kutoharibika vikaja katika mimi kwa ajili ya familia yake ***(2Timotheo 1:10)*** hakuna hata mmoja ambaye angestahili, hakuna ambaye angeweza kulipa gharama kwa maana wote wametenda dhambi na kustahili kifo Yesu pekee ndiye aliyekuwa hana dhambi Kondoo wa Mungu yeye anaoneka anastahili ***(Ufunuo 5:1-6)***.

Yesu Kristo ametuhuisha sisi pamoja nae akiwa ametusamehe sisi maana yetu yote
***(Wakolosai 2:1-2 ; Zaburi 32:1-2)***

Yesu Kristo Mungu ametupatanisha sisi na nafsi yake asituhesabie makosa yetu naye ametupa sisi huduma ya upatanisho ***( 2 Wakorintho 5:18 -20)*** Wayahudi kwa watu wa mataifa yote katika mwili mmoja kwa njia ya Msalaba ***(Waefeso 50:2-16; Warumi 5:10-11)***

Yesu Kristo akiwa amefanya amani kupitia damu yake kwa njia ya msalaba, kwa njiaq yake kupatanisha vitu vyote kwa nafsi yake ***(Wakolosai 1"20 ; Waefeso 2:14-15)***

Kupitia Yesu Kristo tumesamehewa dhambi zetu ***(Waefeso 1:6; Wakorintho 4:1)***
Yesu Kristo ametuokoa sisi kutoka kwenye hofu ya mauti iliyoikabili maisha yetu yote ilitutia kifungoni ***(Waebrania 2:15)*** kama vile Yesu alivyowakomboa Watakatifu wa watu wa kale kutoka jela ya kuzinu akawachukua pamoja nae kwenye utukufu ***(Waefeso 4:7-8) Warumi 8:1-2; Yohana 5:4)*** wale wanaoweza kulikubali lile neno katika ukamilifu wake wako huru kwa sababu lile neno limeshahukumiwa tayari pale msalabani.

Yesu Kristo kupitia mauti yake alimharibu yule aliyekuwa na nguvu za mauti ambae ni shetani ***(Waebrania 2:14)*** kwamba kwa neema ya Mungu aweze kuonja mauti kwa kila mtu
***(Waebrania 2:9)*** nguvu za shetani zimevunjwa.

Yesu Kristo ametakasa dhamiri zetu kutoka kwenye kazi mfu kwa damu yake ambae kupitia Roho wa milele amejitoa mwenyewe bila hatia kwa Mungu, kazi mfu ni kazi tunazozifanya bila ya Mungu ***(Waebrania 9:4; Waebrania 6:1)*** tumeumbwa ndani ya Yesu Kristo kwa akili ya kazi njema ***(Waefeso 2:10; Warumi 4:3-5).***

Yesu Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa wenye dhambi lakini sasa tunahesabiwa haki kwa damu yake na kupitia hili tutaokolewa kwa damu yake ***(Warumi 5:8-9).***

Yesu Kristo aliyejeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yetu na kwa kupigwa kwake sisi tumepona ***(Isaya 53:5-6;1Petro 2:24)*** Yesu alituponya sisi na magonjwa yetu, na maradhi na mateso na huzuni ***(Zaburi 103:3-).***

Yesu Kristo kwa toleo moja aliwakamilisha milele wale ambao wametakasika ***(Waebrania 10:14; Mathayo 5:48)*** kwa hiyo hebu twende katika ukamilifu ***(Waebrania 6:1).*** Yesu Kristo alitukomboa sisi tuliokuwa chini ya sheria kwamba tupokee hali ya kufanywa wana hadi hali kadhalika sisi tulipokuwa watoto tulikuwa watumwa chini ya utaratibu wa dunia ***(Wagaratia 4:1-5)*** sasa tumepokea Roho kufanywa wana ambapo tunalia Aba yaani baba ***(Warumi 8:15)*** sasa sisi tuko kwenye familia ya Mungu ***(Waefeso 1:5 ; Warumi 8:- 23).***

Yesu Kristo ukamilifu kabisa alitimiza sheria ya Mungu kwaajili yetu ili haki ya sheria kutimizwa katika sisi ambao hatutembei kwa kufuata mwili bali kwa kufuata Roho ***(Warumi 8:- 1 - 4).***

Yesu Kristo alitutakasa sisi kwa kuutoa mwili wake uwe sadaka mara moja kwa wakati wote ***(Waebrania 10:- 10; Yohana 17:-16 -19; 1 Wakorintho 1:30 -31)*** waliwatakasa watu kwa damu yake mwenyewe ***(Waebrania 13:12).***

Pamoja na Yesu Kristo tunajua Yule mtu wa kale amesulubiwa pamoja nay eye kwamba mwili wa dhambi uweze kuharibiwa sasa kuanzia sasa tusisumbukie dhambi ***(Warumi 6:6-11)*** ni msemo wa uaminifu usemao kama tumekufa kupitia msalaba wa Kristo, utu wetu wa kale ukiitwa mume wetu wa zamani (wa kwanza ) ***(Warumi 7:1-6)*** umesulubiwa pamoja nay eye mume wetu wa zamani wa kidhehebu, pia ile asili ya dunia ilikufa pamoja naye ***(Wagalatia 6:-14)*** sasa tumeolewa tena na Bwana Yesu Kristo.

Yesu Kristo kupitia damu yake mwenyewe ameandaa njia kwaajili yetu ili tuweze kumfuata yeye tuweze kuingia mahali Patakatifu sana kwa damu ya Yesu ***(Waebrania 10:-19-10).***

Yesu Kristo alitupa sisi uhai wake Mtukufu wa ajabu, uzima wa milele zile chembe za damu za Mungu zilivunjwa pale Kalvari na uhai wake wa Kiungu ukitoka kwenye damu yake walipewa waaminio halisi kwa Roho wake, Ubatizo wa Roho Mtakatifu ***(Yohana 11:- 25 – 26) Yohana 3:-16 ; Yohana 5 :- 24).***

Yesu Kristo kupitia mauti yake pale msabani alitufanya sisi warithi wa Mungu na warithi pamoja na Kristo kupitia mauti yake ya agano ambalo sasa liko linafanya kazi ***(Waebrania 9:15 – 18 ) Warumi 8:17 ; Wagalatia 4: 9).***

Aliye ndani yenu ni mkuu kuliko kile kiti cha magurudumu, aliye ndani yenu ni mkuu kuliko ile machela, alie ndani yenu ni mkuu kuliko ile kansa, aliye ndani yenu ni mkuu kuliko mateso (Ugonjwa) alie ndani yenu ni mkuu kuliko chochote kilichopo mbacho shetani anaweza kuweka juu yenu, amina. Alie ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu''
***( 1Yohana 4:-4)*** aliye ndani yenu ni mkuu, ndiyo yako ndani yetu huyo ni Kristo
***(Warumi 8:37)*** alikuwa ni mshindi wa kila adui alimshinda kila adui kwaajili yetu alipokuwa hapa duniani alishinda dhambi, alishinda magonjwa, kuzimu, mauti, kaburi na amekuja kwetu kutuweka huru kutoka mambo hayo yote, aliye ndani yetu ni mkuu kuliko Yule anayeweza kuweka vitisho ndani yetu ndiyo aliye ndani yetu ni mkuu kuliko Yule aliye katika dunia (6).

Namkemea shetani, shetani wewe sio chochote lakini mtishaji tu na wewe umewekwa wazi hapa kwa ushuhuda wa maandiko ya Yesu Kristo aiishie aliefufuka, ninakuamuru wewe kwa Mungu aliye hai utoke kwa watu hawa na uwaache uende kwaajili ya Utukufu wa Mungu, wote wanaokubali uponjaji wao wasimame kwa miguu yao sasa na waseme ninaamini, haijalishi kuna tokea nini, haijalishi itachua muda gani litaenda kutokea sasa nakubali hilo kwa moyo wangu wote inueni mikono yenu sasa, asanteni, Bwana asifiwe, mpe yeye sifa sasa inueni mikono yenu na mumsifu yeye kwaajili ya uponyaji wenu. (7)

Sasa Bwana himizo limefanyika kwamba shetani yeye mdanganyifu mkuu hana haki ya kuwashikilia watoto wa Mungu yeye ni kiumbe alieshinda ***(Wakolosai 2:13 -15)*** Yesu Kristo alie mahali pekee pa kuabudia jina pekee la kweli limemshinda yeye pale Kalvari kuweka mikono juu ya wagonjwa nao watapata afya ***(Marko 16:17-18)*** tunazungumza hilo katika jina la Yesu Kristo (11).

Baba Mungu maisha yetu yote yamefungwa katika hilo kwa sababu ni wawe na wewe uzima wetu sasa kuna baadhi ya watu hapa bwana ambao wanashikilia hii ishara ambayo tuna zungumza juu yake ameishikilia hiyo ishara na bado ni wagonjwa na wanataka kuzungumza kuwatia moyo kumchukua haki waliopewa na Mumgu wana haki kumshinda shetani yeye amekwisha kushindwa nay eye ni mtishaji tu nina wadai hao baba. (12)

**NUKUU ZA KIINGEREZA**

*(1) Ile ishara (64-0208) aya 161-162*
*(2) Ile isha (63-1128E) aya 167-168*
*(3) Kumita Yesu katika kituko (64-0319) aya 6*
*(4) Mhuri wa Pasaka (65-0319) aya 115-1201128*
*(5) Imani ni ushindi wetu (58-1004) aya 21*
*(6) Alama ya mnyama na mhuri wa Mungu (61-0216) aya e-80*
*(7) Aliye ndani yako (63-1110E) aya 194-195*
*(8) Uwepo wa Mungu usiotambulika (64-0618) aya 235-237*
*(9) Mahali Mungu alipochagua pakuabudia (65-0220) aya 130*
*(10) Sema na huu mlima (57-1215) aya E-28*
*(11) Tuonyeshe baba (61-0521) aya e-110*
*(12) Nyakati (63-091e) aya 40.*

---

Jiwe la kiroho la kujengea No. 1 mpya 2010) kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald
Friedsfr.69,D-75328 Schomberg, Germany
www.biblebelievers, Fax (+49)72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098.*